# Muelekezo Kuhusu Canvas (Kibao cha Mkondoni) kwa Wanafunzi

| | |
|---|---|
| **Ninawezaje kuingia kwenye Canvas?**<br><br>Kuna njia tatu za kuingia kwenye.  Unahitaji tu kutumia moja wapo:<br><br>1. www.fcps.net/canvas<br>2. http://fcps.instructure.com<br>3. Kupitia utaftaji wa Google (1) kwenye Hifadhi yako ya Google, tembeza chini kupata Canvas (2) |  |
| **Ninawezaje kuingia kwenye Canvas?**<br><br>Ndiyo, utatumia anwani yako ya barua pepe ya shule na nenosiri kwa kuingia kwenye Canvas. Itauliza akaunti yako ya Google. (1) **Tumia anwani yako ya barua pepe ya shule na nenosiri.** Usitumie akaunti ya kibinafsi.<br><br>Kumbuka, mwisho wa anwani yako ya barua pepe ni:<br><br>@stu.fayette.kyschools.us |  |
| **Je! Unakubaliana na Matumizi Mazuri ya Sera?** |  |

<table>
<tr><td>Ndio, lazima ukubaliane na Matumizi Mazuri ya Sera mara ya kwanza kuingia mtandaoni. Hii haitajitokeza baada ya kukubaliana na kuwasilisha mara ya kwanza.</td><td></td></tr>
<tr><td>

**Je! Elimu au kozi zangu zapatikana wapi?**

Elimu au kozi zako zaweza kuonekana katika moja ya maeneo haya mawili:

1. Dashibodi (1)
2. Kozi- kozi zote

</td><td>




</td></tr>
<tr><td>

**Kidokezo:** Weka au ondoa nyota kwenye elimu au kozi zote ambazo unataka kuongeza au kuondoa kwa dashibodi yako

</td><td>




</td></tr>
<tr><td>

**Ninawezaje kuingia kwenye Kozi?**

Bonyeza kozi mara mbili kwenye Dashibodi (1) au bonyeza kichwa cha kozi kwenye orodha ya kozi (2)

</td><td>




</td></tr>
</table>

## Mara tu nipo ndani ya darasa langu, nianzie wapi?

Mwalimu wako anaweza kuwa na ukurasa wa utangulizi (1) au orodha ya mitazamo (2) kwa ajili yako.

Fuata maagizo kwenye ukurasa wa utangulizi kutoka kwa mwalimu wako. Orodha ya mitazamo inaitwa **Moduli**. Moduli (2) ni mahali utafanya kazi za kozi yako. Mwalimu wako atakuwa na shughuli tofauti.




**Kidokezo:** Tafuta kitufe kinachofuata ndani ya shughuli ili kuhamia kwa ukurasa unaofuata kwenye Moduli.




## Picha tofauti zilizo katika mtazamo wa moduli zinamaanisha nini?




**Kurasa (1)** - Utapata yaliyomo ndani ya darasa lako kwenye ukurasa huu. Kunaweza kuwa na video za kutazama, au unaweza kupata slaidi za kutazama.

**Kazi (2)** - Utawasilisha kazi zako hapa. Mwalimu wako anaweza kuongeza video na vifaa kadhaa, lakini atakuuliza uwasilishe kitu kwao.

**Bodi ya Mazungumzo (3)** - Mwalimu wako anaweza kukuuliza ushiriki katika

| | |
|---|---|
| mazungumzo ya maandishi kama sehemu ya kazi za shule. Utajadili mada na wenzako wa darasa hapa.<br><br>**Jaribio (4)** - Mwalimu wako anataka kujua unachojua. | |
| **Ninawasilishaje kazi ya shule?**<br><br>1. Fungua kazi<br>2. Soma maelekezo na fuata maagizo<br>3. Unapokuwa tayari, bonyeza kwenye pembe ya juu kwa mkono wa kulia ili (1) kuwasilisha kazi<br><br>4. Kulingana na aina ya kazi, unaweza:<br>a. Kusasisha faili kutoka kompyuta yako au Chromebook (2)<br>• Chagua "Choose File" (Chagua faili)<br>• Chagua Faili ya kazi<br>• Bonyeza "Open" (Fungua)<br><br>b. Shiriki kiunga na mwalimu<br>c. Rekodi Video au Sauti kwa kutumia Media<br>d. Ingiza Hifadhi ya Google au Hati ya Ofisi ya 365 – huenda ikakubidi uruhusu akaunti yako ya Google. Angalia *"Nitaruhusuje* |  |

| | |
|---|---|
| *akaunti yangu ya Google" kwa kupata msaada ?*<br>e. Kamilisha kazi kwa kufungua bidhaa ya Google (3) au kutumia dirisha la hakiki (4).<br><br>5. Mara kazi wako inapokamilika, bonyeza kitufe cha Kuwasilisha Kazi mara moja tena.<br><br>6. Utaona uthibitisho kwenye kona ya juu ya skrini, na itaonyesha wakati na tarehe ya uwasilishaji. | |
| **Kidokezo:** Kumbuka kuangalia tarehe zamwisho wa kuwasilisha kazi, ili usikose kuwasilisha kazi. Tarehe za mwisho wa kuwasilisha kazi zinaonekana kwenye kona ya juu kushoto, chini ya kichwa cha kazi. |  |
| **Je! Nitaruhusuje Akaunti yangu ya Google?**<br><br>1. Bonyeza kitufe "Authorize" (Ruhusu) (1)<br>2. Chagua akaunti ya shule lako (2)<br><br>Itaweza kukubidi uweke anwani yako ya barua pepe ya shule na nenosiri. |  |

| | |
|---|---|
| 3. Chagua “Allow” (Ruhusu) ili Canvas ifikie Hifadhi yako ya Google (3) | <br> |
| **Kuna kalenda?**<br><br>Ndio, chapa ya kalenda (1) inapatikana kwenye baraza ya zana ya upande wa kushoto. Ikiwa mwalimu wako anatumia tarehe za mwisho za kuwasili kazi, kazi hizi zitaonekana kwenye kalenda yako kwa kozi zote. Kalenda ni rafiki yako ili ufanikishe kwenye Canvas. Unaweza pia kubonyeza kwenye kazi (2) ili kuihakiki na kuikamilisha. | <br><br><br> |
| **Je! Ninaweza kumtumia mwalimu wangu ujumbe kupitia Canvas?**<br><br>Ndio, ikoni ya Inbox inakuruhusu kumtumia mwalimu wako barua pepe moja kwa moja. Huna haja ya kwenda kwenye Outlook kwa kutuma barua pepe kwa mwalimu wako.<br><br>1. Fungua Inbox (1) | <br> |

<table>
<tr>
<td>

2. Bonyeza kitufe cha “Compose” (kutunga) (2), kwenye mkono wa kulia juu
3. Chagua kozi yako
4. Chagua mwalimu wako (3)
5. Tunga barua pepe
6. Bonyeza “Send” (Tuma)

</td>
<td>




</td>
</tr>
<tr>
<td>

**Kidokezo:** Kumbuka barua pepe ni rasmi na haipaswi kutumia lugha isiyo rasmi, kama vile ujumbe wa maandishi kwa rafiki yako.

</td>
<td></td>
</tr>
<tr>
<td>

**Je! Kuna app (programu) ya Canvas?**

Ndio, Canvas ina programu ya Mwanafunzi. Unapaswa kupata program katika Duka la Google Play na Duka la App ya Apple. Tafuta: Canvas Student (Canvas ya Mwanafunzi)

</td>
<td>

STUDENT

GET IT ON Google Play

Available on the App Store

</td>
</tr>
<tr>
<td>

**Je! Ninawezaje kuanzisha Programu ya Mwanafunzi?**

1. Pakua programu **Canvas Student** kutoka duka lako la programu.
2. Fungua programu ya Canvas Student.

</td>
<td>




</td>
</tr>
</table>

<table>
<tr>
<td>

3. Bonyeza kitufe ya “Find School” (Kupata Shule) (1)
4. Ingiza: **fcps.instructure.com** <u>SIYO</u> Fayette County
5. Chagua Wanafunzi na Wafanyakazi wa FCPS- (KY) (2)
6. Ingia na anwani yako ya barua pepe ya FCPS na Nenosiri (3)
    a. Kumbuka, anwani yako ya barua pepe inamalizika na: @stu.fayette.kyschools.us

</td>
<td>




</td>
</tr>
<tr>
<td>

**Kidokezo:** Ruhusu Arifa, kwa hivyo unaweza kujulishwa wakati mwalimu wako atafanya chapisho mpya au tangazo.

</td>
<td>




</td>
</tr>
<tr>
<td colspan="2">

## Je! Ninahitaji Programu ya Canvas Student?

Programu inapatikana ili uwe nayo kwenye vifaa vyako vya kibinafsi. Matumizi yake **hailazimiki**. Inashauriwa kutumia programu tu kwa habari za haraka lakini kwa kufanya na kumaliza kazi, tumia Chromebook yako. Programu ni kifaa cha ziada kukusaidia kufanikiwa.

</td>
</tr>
<tr>
<td colspan="2">

## Dawati ya Msaada wa Wanafunzi na Familia

</td>
</tr>
</table>

Wanafunzi na familia ambazo zinapata maswala ya kiufundi na vifaa vilivyotolewa na wilaya au wakiwa na shida ya kupata mtandao wanaweza kupata msaada kutoka kwa Dawati la Msaada wa Wanafunzi na Familia.

Nambari ya Simu: 859-381-4410

Siku na Saa kwa Mwaka wa Shule: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 2 asubuhi hadi 2 usiku